

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA WILAYA YA MAKETE

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

SHULE YA SEKONDARI MLONDWE.

KUMB. NA: MLD/S.2029/FJ/ 2021

JINA LA MWANAFUNZI.....

NAMBA YA MTHANI.....

NAMBA YA SIMU.....

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MLONDWE.

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa bodi ya uchaguzi imekuchagua kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari mlondwe. Ni mategemeo ya jumua ya mlondwe sekondari kuwa utaikubali na kuitumia vizuri nafasi hii nyeti uliyopewa.

Unapoipokea nafasi hii kumbuka kuwa ushirikiano wako na wanafunzi wenzako, walimu, mkuu wa shule pamoja na wafanyakazi wote juhudi na maarifa vikiwa vimejengwa juu ya NIDHAMU ndio siri ya mafanikio yako.

Ukifika shuleni unatakiwa kuonana na Mwalimu mwandamizi Malezi kwa maelezo zaidi.

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**

MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI.

A: SARE ZA SHULE

WAVULANA.

1. Aje na suruali mbili za rangi ya Dark blue moja na Kijani Mgomba moja
2. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu (Tetroni)
3. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba ndefu visivyo na kisigino jozi mbili.
4. Soksi nyeusi jozi mbili
5. Sweta la blue
6. Tai mbili kufuatana na rangi za suruali zote mbili.
7. Traksuti mbili zenye mkanda mweupe, moja nyeusi na moja ya blue
8. Blanketi moja
9. Shuka (2) blue bahari
10. Godoro moja 2.5 kwa 6
11. Aje na Koti moja jeusi fupi la kuvaa wakati wa baridi

NB:

1. Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa.
2. Aje na nguo za ndani za kutosha.

WASICHANA.

1. Aje na sketi mbili za rangi ya Dark blue moja na Kijani Mgomba moja mshono wa marinda ya kumwaga.
2. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba ndefu visivyo na kisigino jozi mbili
3. Mashati mawili meupe mikono mirefu (Tetroni).
4. Soksi nyeupe jozi mbili.
5. Sweta la blue moja
6. Tai mbili kufuata rangi za sketi
7. Traksuti nyeusi mbili zenye mkanda mweupe
8. Blanketi moja
9. Shuka (2) la pinki
10. Godoro moja 2.5 kwa 6
11. Sketi mbili za blue bahari mshono wa soro
12. Aje na Koti jeusi moja fupi la kuvaa wakati wa baridi

NB:

1. Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa.
2. Aje na nguo za ndani za kutosha.

B: VIFAA VYA KITAALUMA.

1. Daftari kubwa 10(Counter book)
2. Bic, begi moja la kubebea daftari na rula
3. Zana za Hisabati (Mathematical set/Mkebe)
4. Kamusi moja ya Kiswahili na moja ya kiingereza.
5. Aje na sanduku la chuma.
6. Aje na faili la kutunzia kumbukumbu zake
7. Aje na fedha Sh. 14,000/= kwaajili ya mwalimu wa sayansi

C: VIFAA VYA USAFI WA BINAFSI, BWENINI NA MAZINGIRA .

- Mwanafunzi aje na;
 1. Ndoo mbili, Kubwa moja na Ndogo
 2. Kwanja moja
 3. Jembe jipya
 4. Mopper kifaa cha kudekia.

D: MAHITAJI YA CHAKULA.

- Mwanafunzi anatakiwa aje na;-
 1. Mahindi debe sita (6) kwa mwaka.
 2. Maharage debe mbili (2) kwa mwaka.
 3. Fedha shilingi Laki moja na elfu tano kwa mwaka (105,000/=)Kwa ajili ya kununulia bidhaa za chakula za dukani pamoja na kuwalipa wapishi na matroni.
 4. Lazima mzazi ukamilishe nusu ya michango unapomleta mwanao shuleni.
 5. Aje na fedha Sh. 22500/= mchango wa kununua mashine ya kusaga nafaka.

ANGALIZO:

MWANAFUNZI ASIYETIMIZA NUSU YA MCHANGO WA CHAKULA CHAKE HATAPOKELEWA KWA KUWA LAZIMA MWANAFUNZI APATE CHAKULA SHULENI. MZAZI TIMIZA WAJIBU WAKO.

E: SHERIA ZA SHULE.

Zifuatazo ni baadhi ya sheria za shule hii.

1. Ni kosa kubwa kutohudhuria vipindi darasani bila sababu yeyote.
2. Kuchelewa kufika shuleni siku ya kufungua shule ni kosa
3. Kunywa pombe , kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya ni kosa kubwa
4. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu, radio au silaha.
5. Wizi , uzinifu, ugomvi, matusi utapeli, uasherati na uhusiano wa kimapenzi na kutoa au kusababisha mimba ni kosa kubwa na haviruhusiwi kabisa kufanywa na mwanafunzi yeyote
6. Mwanafunzi lazima avae sare ya shule wakati wa kwenda likizo na wakati anarudi kutoka likizo.
7. Ni kosa kubwa mwanafunzi kukwepa kufanya mazoezi, majaribio na mitihani mbalimbali ya kitaaluma.
8. Ni kosa kubwa kuwa katika jozi ya kike na kiume.
9. Kila mwanafunzi lazima awe mtiifu kwa walimu, wafanyakazi, viranja wa shule na wakubwa wengine.
10. Ni marufuku kupanda kitandani wakati wa mchana, Ukipatikana utachonga kitanda kipya.

KARIBU SANA MLONDWE SEKONDARI.

.....

MKUU WA SHULE.

NAMBA: 0757 734804.